

BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inatarajia kukusanya/kupokea fedha kiasi cha **Tsh. 138,701,780,500.00** Kati ya fedha hizo **Tsh. 86,776,429,500.00** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu, **Tsh 44,672,948,000.00** ni fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri, na kiasi cha **Tsh.7,252,403,000.00** ni kutoka TAMISEMI kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara (Road Fund).

JEDWALI 1: MUHTASARI WA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018

RUZUKU ZA SERIKALI	MAPATOYA NDANI	MFUKO WA BARABARA	JUMLA
86,776,429,500.00	44,672,948,000.00	7,252,403,000.00	138,701,780,500.00
63%	32%	5%	100%

JEDWALI NA. 2: MHUTASARI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO

VYANZO VYA NDANI	MCHANGO WA WANANCHI	RUZUKU KUTOKA S/KUU	MFUKO WA BARABARA	JUMLA
26,803,769,000.00	686,380,000.00	29,397,105,500.00	7,252,403,000.00	64,139,657,500.00
42%	1%	46%	11%	100%

Kiasi cha **Tsh.86,776,429,500.00** za ruzuku kutoka Serikali Kuu kinajumuisha kiasi cha **Tsh.54,907,457,000.00** ikiwa ni mishahara, kiasi cha **Tsh. 2,471,867,000.00** ni matumizi ya kawaida na kiasi cha **Tsh. 29,397,105,500.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo toka Serikali Kuu.

Aidha, Halmashauri inatarajia kupokea kiasi cha **Tsh.7,252,403,000.00** ambayo ni ruzuku kutoka mfuko wa matengenezo ya barabara - TAMISEMI (Road Fund).

Mpango huu umelenga katika kufikia dhima na dira ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

- A) Huduma ya ukimwi kuboreshwa na maambukizi mapya kupunguzwa
- B) Uboreshaji, uendelezaji na utekelezaji kikamilifu mpango wa Taifa wa kupambana na rushwa.
- C) Kuimarika kwa upatikanaji na ubora wa huduma za jamii
- D) Kuongezeka na kuboreka kwa huduma za kiuchumi na miundombinu
- E) Kuimarika kwa utawala bora na utoaji wa huduma
- F) Kuimarika kwa uwezo wa kiuchumi na kijinsia na ustawi wa jamii
- G) Kuimarika kwa usimamizi wa kujikinga na maafa na milipuko ya magonjwa
- H) Kuimarika kwa usimamizi wa maliasili na mazingira

- **TAMKO LA MHESHIMIWA MSTAHIKI MEYA**

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni katika kuboresha maisha ya wakazi wake, imeandaa mpango wa mwaka **2017/2018** na mpango wa muda wa kati **2017/2018 – 2019/2020** unaolenga kukuza uchumi, na kupunguza umaskini ili kufikia maendeleo endelevu ya kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa wananchi wake. Mpango huu umezingatia Ilani ya uchaguzi wa Chama tawala **2015 – 2020**, Sera na miongozo ya Taifa na Dira ya Maendeleo ya Taifa **2025**, Malengo ya Millenium **2015**, Mpango wa Tekeleza Kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), Mpango mkakati wa Manispaa ya Kinondoni wa **2016/2017 - 2020/2021** na mipango shirikishi jamii iliyoibuliwa katika Kata na Mitaa (O&OD).

Aidha ili kutekeleza dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka, mpango huu umeshirikisha jamii, katika mpango shirikishi ambao huanzia ngazi ya Mtaa. Hali hiyo imezingatia vipaumbele na mahitaji halisi ya wananchi katika maeneo yao. Mpango umejielekeza katika kutoa kipaumbele maeneo yanayoweza kutoa matokeo ya haraka (quick wins) ambayo yatasaidia ukuaji wa uchumi kwa haraka katika kipindi kifupi.

Aidha maeneo tuliyoyapa kipaumbele katika mpango huu ni pamoja na:-

- I. Kuboresha na kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Manispaa.
- II. Kuboresha miundombinu ya Afya, Shule za Msingi na Sekondari.
- III. Kuboresha miundombinu ya maji, umeme, barabara na Kilimo mjini.
- IV. Kuboresha hifadhi ya mazingira na ukusanyaji wa taka.
- V. Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- VI. Kuboresha mazingira ya wafanyabiashara ndogondogo.

Ili kuyafikia mafanikio yaliyotajwa hapo juu, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itasimamia yafuatayo:-

- I. Kuimarisha mahusiano mazuri kati ya Serikali, mashirika yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine.
- II. Kuendelea kujenga uwezo na ujuzi kwa watumishi katika utoaji wa huduma zilizo bora na haraka.
- III. Kuimarisha Utawala bora, Uwajibikaji na Uwazi.
- IV. Kujenga uwezo kwa viongozi wakiwemo Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa katika kusimamia shughuli za wananchi.

Mpango wa muda wa Kati wa Matumizi na Bajeti ya mwaka **2017/2018** ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya **Chama tawala ya mwaka 2015 – 2020**. Hivyo matokeo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii yameelekezwa katika kujibu matarajio ya watu ambayo ni utatuzi wa kero zao pamoja na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Benjamin Kawe Sitta
MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

